

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa  
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## TUMEITWA ILI KUTUMIKA

Katika siku tunazoishi kuna haja kubwa ya kuwa na Wakristo ambao ni watumishi waaminifu kanisani. Kuna mahitaji mengi ya maisha ya kila siku katika kanisa la Kristo, na hata kuna mahitaji ya kiroho ambayo yatahitaji kushughulikiwa. Kuna sadaka ambazo zinahitaji kukusanywa na kugawiwa kwa sehemu ambazo kuna mahitaji kanisani. Pia kuna miradi ya kuosha kanisa na hata kuidumisha katika hali bora. Kuna sherehe ambazo zinahitaji kupangwa, wagonjwa ambao wanahitaji kutembelewa, na hata masikini ambao wanahitaji kusaidiwa. Basi ni jambo la baraka kubwa kwa mwili wa Kristo kama kutakuwa na watumishi waaminifu ambao wanaweza kufanya kazi bila kuchoka, bila hata kujitangaza, na ambao watafanya kazi hiyo kwa njia ya kujitolea kabisa.

Hali bora ya kiafya ya washiriki wa kanisa na maendeleo yao ni mambo ambayo hayategemei tu kazi ya mchungaji na huduma yake, bali pia hutegemea kuwepo kwa watumishi ambao ni waaminifu kanisani. Katika makusanyiko mengi ya kanisa mzigo wa maisha ya kila siku ya washirika, na hata ule wa mambo ya kiroho hubebwa tu na wahudumu au wachungajiwa kanisa hilo. Lakini ikiwa wachungaji watajihusisha sana na mambo ya kila siku ya washirika wao, basi watumishi hao hawatabakisha uwezo wa kiakili na nguvu za mwili za kujitolea mhanga katika kazi yao ya kiroho. Basi ukweli ni kwamba, washirika wa kanisa wana jukumu na mweke wa kujitolea kama watumishi wa kanisa. Bwana wetu Yesu Kristo ndiye alituachia mfano bora wa utumishi, "Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Marko 10:45).

Jinsi ambavyo nyumba zetu za kibinafsi zinahitaji kutunzwa na kudumishwa katika hali bora, ndivyo ambavyo jengo la kanisa

linahitaji kutunzwa. Wakati mwingi kazi ya Injili hainendi kulingana na jinsi inavyopasa kwa sababu mahitaji ya maisha ya kila siku ya kusanyiko la kanisa hayako katika hali bora. Je, si ni jambo bora sana kuona watu wa kila umri wakichukua majukumu katika mwili wa Kristo huku wakitumika kwa ajili ya manufaa ya kanisa. Majengo ya kanisa ambayo yaonekana kutunzwa vizuri, na mambo ya kanisa ambayo yaonekana kuendeshwa vizuri, huwa ni ushuhuda mkubwa kwa ulimwengu.

1 Wakorintho 4:2 inasema: "Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu." Mungu hajawakabidhi watu wake injili tu ya kiroho, bali pia amewapatia kazi ya kutumika na kuhudumu ili kukutana na mahitaji ya wenzao kanisani. Ni jambo rahisi watu kujitolea kazini mwa Mungu muda baada ya mwingine, lakini ni jambo tofauti kabisa kwa watu kujitolea kazini humo kwa uaminifu mkubwa huku wakitumika mwezi baada ya mwingine bila mtu yeyote kuwatambua kwa kiwango kikubwa. Watakatifu wa Mungu wameitwa ili kumfanyia Bwana wao kazi; hii ni kumaanisha kwamba kutosheleka kazini mwa Bwana ni jambo ambalo linahitaji kuwa limetokana na nia ya ndani ya kutaka kumpendeza Mungu, wala sio kutaka kutambuliwa na wanadamu. Kazi ya mtumishi sio kazi ya kifahari, bali ni kazi ya kumpendeza Yeye ambaye anatumikiwa.

Ikiwa ni shemasi au ni mdhamini wa kanisa, ikiwa ni mwalimu wa shule ya Jumapili au kiongozi wa nyimbo, au iwe ni mwimbaji wa nyimbo shesheli, mpikaji, mwangalizi wa jengo la kanisa, au mshirika wa kawaida wa kanisa – kuna haja kubwa ya kuwemo kwa watumishi waaminifu ambao wanaweza kutegemewa na viongozi wa kanisa kwamba watafanya kazi ambayo inahitaji kufanywa kanisani. Huduma ambayo washirika

(Endelea katika Ukurasa 2)



“Hali bora ya kiafya ya washiriki wa kanisa na maendeleo yao ni mambo ambayo hayategemea tu kazi ya mchungaji na huduma yake, bali pia hutegemea kuwepo kwa watumishi ambao ni waaminifu kanisani.”

Viwango Ambavyo  
Biblia Imeweka  
Kuhusiana Na  
Kuhitimu Kwa  
Mashemasi

2

Tahari  
Wahudumu Wa Injili  
Na Swala La Pesa

3

Ofisi Ya Shemasi

4

Maswali na Majibu

7

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa  
Msimu Huu

8

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

## Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

## Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

## Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

## Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,  
Efe. 2:1, 5-6

## Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

## Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

## Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,  
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

## Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

## Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,  
Kol. 1:18

## Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

## Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,  
Yn. 13:14-17

## Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

## Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,  
I Kor. 7:10-11

## Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

## Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,  
Mt. 25:31-46

## Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

## Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

## Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

wanaweza kutegemea, na kuwemo kwa watu kanisani ambao wako tayari kujitoa ili mambo ya kanisa na mahubiri ya Injili yaende vizuri, ni mambo ambayo huwa ni baraka kubwa kwa hali ya afya ya kanisa. Mungu amebariki watu wake na talanta tofauti tofauti, na hata elimu tofauti tofauti. Basi kanisa lingekuwa na mahitaji machache sana kwa mambo ya maisha ya kila siku, na hata yale ya kiroho, ikiwa watu wangejitolea kwa kiwango kikubwa na kutoa talanta zao kwa ajili ya kazi ya Mungu. Furaha na baraka za Mungu ni mambo ambayo hupatikana kutokana na mtu kujitoa mhanga kwa ajili ya utumishi wa maisha yake na hata mali yake kwake Bwana.

Hebu inua macho yako ili uweze kuona kazi ambayo imekuzunguka, na ili uweze kujitoa kwa uaminifu kumtumikia Bwana wako. ■

## Viwango Ambavyo Biblia Imeweka Kuhusiana

# NA KUHITIMU KWA MASHEMASI

(Kutoka 1 Timotheo 3:8-13 na Matendo 6:3)

- Watu waliojazwa Roho Mtakatifu.
- Wastahivu.
- Sio walevi.
- Watu wenye ukweli na wenye kuaminiwa. Sio watu hadaa.
- Wasio na tamaa ya pesa.
- Watu wanaoamini na kuishi kulingana na mafundisho ya ukweli.
- Waaminifu.
- Waliojaribiwa na kuhitimu. Sio waongofu wanya bali watu wenye ujuzi.
- Wenye hekima.
- Watu wenye ushuhuda na sifa za kuishi kwa ukweli.
- Watu wasio na lawama.
- Mume wa mke mmoja aliye hai (kuoa wake wengi na pia uzinzi ni mambo ambayo yamekatanzwa).
- Wake wao wawe watu wenye kiasi, wenye heshima, waaminifu, watu wasiosingizia wale wengine.
- Watoto wao wawe watiifu.
- Nyumba yao iwe ambayo imetunzwa vyema na yenye utaratibu.

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya [www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org) na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA  
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



“Wale ambao ni mashemasi wa maajabu ya Kristo hawana budi kupendeza watu wote kwa kila njia. Hii ni kwa sababu wao sio tu mashemasi wa chakula na kinywaji, bali pia ni watumishi wa kanisa la Mungu” (*Waraka wa Ignatius*, aliowaandikia watu wa Trallians, katika karne ya pili).

Somo letu katika robo hii ya mwaka linahusiana na ofisi au kazi ya mashemasi. Hili ni somo muhimu kabisa, na mimi mwenyewe nimekwisha shawishika kwamba kama kazi ya shemasi ingeeleweka vizuri na kuchukuliwa kwa umuhimu wake, kazi yote ya injili ingeendelea vizuri zaidi, nayo makusanyiko ya Wakristo yangalikuwa katika hali bora zaidi. Lakini ni wakati tu nilipojitumbukiza ndani zaidi kulitafiti jambo hili ndipo nikatambua kwamba hili ni somo ngumu. Baadaye nikawa nasoma kutoka kwa kitabu cha *Kanisa la Mitume (The Apostolic Church)* nikafika mahali ambapo ilimbidi C.E. Brown kufanya uamuzi kama wangu, aliposema kwamba: “Huenda ikawa somo kuhusu kazi au ofisi ya shemasi ndiyo sehemu ngumu zaidi kueleweka kati ya sehemu zote ambazo zinahusiana na katiba ambayo ilifuatwa na kanisa la kwanza.”



Tutembelee

[www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org)

ili kujiandikisha na

kupata jarida

za mbele.

Shida hii imetokana na ukweli kwamba kuna mambo machache sana ambayo yamesemwa katika biblia kuhusiana na ofisi hii, basi inatubidi tuchanganye usomi wetu wa Maandiko kadhaa wa kadhaa yanayohusu mashemasi pamoja na historia ya kanisa ili tuweze kuelewa jambo hili vizuri. Mashemasi ni watu muhimu katika kuendelea vizuri kwa Kanisa la Mungu. Hata ingawa watu wote wameitwa ili watumike, ni dhahiri kwamba kuna watu wengi ambao wanatumika kufanya kazi ya mashemasi katika makusanyiko mengi ya Kikristo na ambao hawajawekwa wakfu kwa kazi hiyo ya ushemasi. Watu hawa ni wale ambao wako na mwito maalumu (wa Mungu) wa kutumika kanisani, na pia ambao wana uongozi wa kiroho ambao ni zaidi ya wajibu wa mtu kufanya kazi kanisani kama mdhamini au mweka hazina wa kanisa. Kuna washirika wachache ambao ni waaminifu, na ambao hawakomi kufanya kazi ya Bwana na kutia bidii kazini, wakitumika kwa ajili ya mambo ya maisha ya kila siku ya kanisa, na hata kusaidia na kuunga mkono kwa mambo ya kiroho. Jina hili shemasi hutumika kusimamia mambo tofauti tofauti katika madhehebu tofauti tofauti, lakini kuna umuhimu wa kutambuliwa kwa wito wa Mungu kwa ajili ya ofisi hii ya shemasi, kwenye kanisa la mahali moja, wito ambao hutokana na Mungu. Sisi sote tunahitaji kuelewa jambo hili kulingana na jinsi limeelezwa katika Maandiko. Lakini hakuna haja ya sisi kuchanganyikiwa, kanisa lake Mungu haliendeshwi kulingana na misingi ya vyeo; ndiposa halina cheo maalum cha mashemasi. Cha muhimu mno kwa ofisi hizi ni utumishi wa Mungu, sio swala la vyeo, kutambuliwa, au wadhifa wa mtu. Basi la muhimu zaidi kuliko ofisi ni roho ya unyenyekevu na upendo maishani mwa watumishi wa Mungu.

Hata ingawa mafundisho ambayo yanafaa kuhusiana na mashemasi yalipotea kutokana na kuanguka kwa kanisa kuacha ukweli, na pia kwa ajili ya taratibu za kanisa Katoliki (la Kirumi) ambalo liliendeshwa kwa misingi ya kibinadamu, ukweli ni kwamba ofisi ya mashemasi imekuwa sehemu ya kanisa la Mungu tangu wakati wa mitume. Ni jambo muhimu kwamba mafundisho kuhusu ofisi hii na kufanya kazi kwake kuendeleo kudumu kanisani. Watu wengi hawaelewi ofisi hii vizuri. Wengi hudhani kwamba ofisi hii inastahili kushikiliwa na wazee vikongwe ambao wamedumu kanisani kwa miaka mingi, ambao huendelea kushikilia mamlaka yao kanisa; kwa sababu ni ukweli kwamba wakati unapofika wa mchungaji kuacha kazi kanisani mashemasi ndio huendelea kudumu uongozini. Lakini shemasi ni mtumishi (wa Mungu) ambaye huendelea kusaidia kanisa kwa uaminifu kwa maswala ya maisha yake ya kila siku, na hata pia ni mtu mwenye kujenga Wakristo kiroho. Mashemasi wanahitaji kuwa watiifu kanisani wanakotumika, na pia wanahitaji kuwa na heshima kwa watu wale wengine, huku wakitumikia Bwana kwa unyenyekevu. Shemasi mzuri ni mtu ambaye anaweza kutegemewa, mwenye bidi, na ambaye ni mfano bora wa utumishi kanisani kwa washirika wale wengine wa kanisa.

Maombi yangu ni kwamba Mungu atabariki Kanisa la Mungu ili liweze kuelewa zaidi ukweli kuhusu ofisi ya shemasi na wajibu wake.

Michael W. Smith, Oktoba 2020.

## Wahudumu Wa Injili wa SWALA LA PESA



Mitume wa Yesu waliambia kusanyiko la kanisa la Yerusalemu kuchagua wanaume saba ambao wangeshughulikia maswala ya kifedha ya kanisa. Jambo hili lilifanyika wakati washirika wa Kiyunani walipoanza kunungunika kwamba hawakuwa wakitendewa usawa kwa swala la ugawaji wa chakula. Hata ingawa wakati mwingine jambo hili haliwezekani, ni jambo la busara kwa mhudumu wa injili kutokuwa pia ndiye mdhamini wa kanisa, asiwe ndiye mwenye kusimamia maswala ya kifedha ya

kanisa lake, ili yeye aweze kuepuka mitego ya adui. Kwa kuepuka kazi hizo yeye ataweza kufanya kazi yake ya kuhubiri kanisani bila kuzingatia ni mshirika yupi anamuunga mkono kwa mambo ya kifedha. Kwa kufuata utaratibu wa Maandiko wachungaji wanastahili (kwa kiwango kile ambacho kinawezekana) kuwaruhusu watu ambao wana ushuhuda bora katika kusanyiko lao kushughulikia maswala yote ya kifedha mle kanisani.

# OFISI YA SHEMASI

Hata ingawa ni kweli kwamba kuna vipawa vingi vya kiroho, ofisi ya askofu na ile ya shemasi ndio ofisi rasmi ambazo zinaonekana kwenye biblia katika kanisa la Agano Jipya. Ofisi hizi mbili ndizo huwajibika kwa uongozi wa kanisa na hizo hufanya kazi yake chini ya mamlaka ya Roho Mtakatifu (1 Timotheo 3:1,8).



“Shemasi ni mtu ambaye yu tayari kuwatumikia watu wale wengine, kuwapakulia chakula, mhudumu, mtumishi.”

Katika maandiko afisi ya askofu ni kitu kimoja na ile ofisi ya mzee wa kanisa, na haya ni majina ambayo yametumiwa kuwakilisha watu ambao wameitwa na kuhitimishwa kuwa wauhubiri wa Neno la Mungu. Kuna ushahidi mwingi wa kuonyesha kwamba ofisi ya maaskofu na ile ya wazee wa kanisa zilikuwa kitu kimoja, na kwamba ni wakati ambapo tu Kanisa la Katoliki la Kirumi lilipoanguka na kuacha na ukweli ndipo ofisi hizi mbili zilitofautishwa.

Nayo ofisi ya daraja la pili ni ile ya shemasi. Mashemasi ni viongozi ambao wanahudumu ili kukutana na mahitaji ya kila siku ya kanisa, na pia ambao wanawasaidia wazee. Lakini viwango vya kuhitimu ambavyo vinahitajika kwa mashemasi ni kama zile zinazohitajika kwa ofisi za maaskofu, isipokuwa kwamba wao hawahitajiki kuwa na “uwezo wa kufundisha.” Ofisi hii ya shemasi ni ofisi ambayo imeamuriwa na Mungu, na inahitaji kushikiliwa na watu ambao wamehitimu kiroho.

## Imetajwa kwa Njia Ambayo si ya Moja kwa Moja

Sisi kujifunza kuhusu ofisi ya shemasi kwa njia ya Maandiko ni jambo ambalo laweza kuwa na ugumu na ni jambo ambalo linaweza kumchanganya mtu. Hii ni kwa sababu hata ingawa Biblia inasema kuhusu ofisi hii na viwango vya kibiblia ambavyo vinahitajika ili mtu ahitimu kutumika katika ofisi hiyo, Biblia yenyewe haisemi kwa mapana na marefu kuhusu kazi zote ambazo zinahusu ofisi hii, na pia haineni kuhusu cheo chake katika uongozi wa kanisa. Ni kweli kwamba Mungu hujali zaidi kuhusu tabia za shemasi, hata kuliko wajibu wa ofisi yenyewe. Ni ni jambo muhimu kuzingatia kwamba kazi ya ofisi hizi mbili zinahitaji kuchukuliwa kwa vipimo sawia, bila watu kuzua maswala ya vyeo vya utawala, ambavyo vimekiuka ya mfano ambao tumepewa na kanisa la mitume. Basi ni muhimu sana sisi kujifunza kwa umakini

mambo ambayo Biblia imesema kuhusiana na swala hili, na kulichunguza kwa mwanga wa historia ya kanisa, huku tukizingatia mahitaji ya maswala ya kila siku ya kanisa la sasa, na hata mahitaji ya kiroho ya washirika wake.

## Maelezo ya Maana

Shemasi ni neno ambalo limetafsiriwa kutokana na neno *diakonos* na ambalo chanzo chake ni lugha ya Kiyunani. Maana ya neno hilo ni mtu ambaye yu tayari kuwatumikia watu wale wengine, ambaye yu tayari kuwapakulia chakula mezani, mhudumu, mtumishi (*Kamusi ya Kiyunani ya Strong na ile ya Thayer*). Neno hili *diakonos* limetumika zaidi ya mara 30 katika Agano Jipya, lakini likatafsiriwa kwa njia tofauti tofauti. Mara nyingi neno hili halitumiki kuonyesha ofisi rasmi ya shemasi. Hebu tutazame maandiko kadhaa ili tuweze kufafanua jambo hili vizuri. Mathayo 20:26 inasema, “Bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi [*diakonos / shemasi*] wenu.” Warumi 13:4 inasema kuhusu viongozi wa kiserikali na kuwaita wahudumu [*diakonos / shemasi*]. Mtume Paulo naye akanena na kusema yeye alifanywa “mhudumu [*diakonos / shemasi*] wake, kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa” (Waefeso 3:7). Neno *diakonos* limetafsiriwa kama “mtumishi” katika maandiko tofauti tofauti. Mathayo 23:11 inasema “Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi [*diakonos / shemasi*] wenu.” Hata watumishi wa mfalme, ambao walitumikia mezani, walijulikana kama *diakonos*/mashemasi, kama ambavyo inaonekana katika Mathayo 22:13 na Yohana 2:9. Basi ni dhahiri kwamba neno *diakonos* lilitumiwa kuonyesha utumishi na huduma wa aina tofauti tofauti; sisi watakatifu tumeitwa ili tuwe wahudumu na watumishi wanaotimiza wajibu tofauti tofauti kanisani.

## Afisi ya Shemasi

Neno *diakonos* lilipata maana zaidi wakati mtume Paulo alihutubia kanisa la Filipi, hapo karibu mwaka 62 BK. “Kwa watakatifu wote

katika Kristo Yesu, walioko Filipi, pamoja na maaskofu na mashemasi [*diakonos*]” (Wafilipi 1:1). Mtume Paulo alihutubia watakatifu hao na kutaja ofisi hizo mbili tofauti, ofisi ya askofu (wazee wa kanisa) na ile ya mashemasi. Salamu hizi ni muhimu na zinatwezesha kuelewa mipango na afisi ambazo zilikuwako katika makanisa ya kwanza ya Kristo. Udhambi na kutambulika kwa ofisi hii ya shemasi kunapatikana zaidi wakati mtume Paulo aliandika katika 1 Timotheo 3 kuhusu viwango vya kufuzu ambavyo vinatajikana kwa wale ambao watatumika katika ofisi hizo: “mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema. Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika . . . vivyo hivyo mashemasi [*diakonos*] na wawe . . .” Ni dhahiri kwamba kufikia wakati mtume Paulo alikuwa akiandika tayari kulikuwa na ofisi spesheli na wadhifa spesheli wa shemasi, na ilikuwa ofisi ambayo ilikuwa zaidi ya utumishi wa kawaida katika mwili wa Kristo.

### Umuhimu wa Ofisi Hii

Kwa sababu sasa tumeonyesha kwamba mashemasi walikuwako katika kanisa la mitume, basi swali lililobaki ni, “Je, kusudi la kuwepo kwa ofisi ya shemasi ni ipi?” Hata ingawa maandiko hayajatuweza jambo hili bayana, tunaweza kupata habari zaidi kutokana na mifano inayopatikana katika biblia. Wajibu spesheli ambao watumishi wa Kristo walikuwa nao ulikuwa wa kuhubiri injili, lakini pia Kristo aliwafundisha wanafunzi wake kuwahudumia maskini, na pia kukutana na mahitaji ya kila siku ya waliokuwa na mahitaji. Ni dhahiri kwamba Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakiungwa mkono kwa kiwango fulani na matoleo ya watu wengine (Luka 8:3). Ndiposa kukawa na haja ya kuwe na mtu wa kupanga fedha na matoleo ya waliomuunga Kristo mkono. Inaonekana kwamba Yuda ndiye alipewa kazi ya kubeba hazina ya pesa (Yohana 12:4-6), na alikuwa na wajibu wa kununua vitu ambavyo vilihitajika, na pia kusimamia matoleo yao kwa maskini (Yohana 13:29). Jambo hili ni dhahirisho la haja ya kuwa na mtu ambaye atasimamia na kupanga mambo ya kifedha ya kanisa.

### Kuchaguliwa ili Watumike

Baada ya siku ya Pentekote kanisa liliweza kukua kwa haraka na mitume hawakuhubiri injili peke yake, bali pia walishughulikia maswala ya kifedha ya kanisa. Huenda ikawa mambo ambayo yanaonekana katika Matendo 6:1-6 ndio yalizua haja ya ofisi ya shemasi kanisani.

Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeka hesabu yao, palikuwa na manung’uniko ya Wayahudi wa Kiyunani juu ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahauliwa katika huduma ya kila siku [*diakonia/ushemasi*]. Wale thenashara wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema, Haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumu mezani [*diakoneo/shemasi*]. Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia [*diakonia/ushemasi*] lile Neno. Neno hili likapendeza machoni pa mkutano wote; wakamchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho

Mtakatifu, na Filipo, na Prokoro, na Nikanori, na Timoni, na Parmena, na Nikolao mwongofu wa Antiokia; ambao wakawaweka mbele ya mitume, na walipokwisha kuomba wakaweka mikono yao juu yao.

Watu hawa walipewa jukumu la kutunza watu kwa mambo ya chakula, pia wakafanywa wasimamizi wa mambo ya kifedha na mahitaji ya kila siku ya kusanyiko la Yerusalemu, ambalo liliendelea kukua kwa haraka. Hata ingawa maandishi ya kale yalisema kwamba watu hawa ndio walikuwa mashemasi wa kwanza (*yale ya Ireneus wa karne ya pili*), Luka akiandika katika Matendo ya Mitume amewaita watu hawa mashemasi kwa njia ambayo ni ya moja kwa moja. Ndiposa kumezuka mgogoro wa kihistoria na kithiolojia ambao ungali waendelea hadi sasa kuhusiana na swala hili. Ni jambo la kuzingatia kwamba kanisa lilikuwa likikua kwa haraka sana wakati huu. Na ni kweli kwamba hali ambayo inaonekana katika Mitendo 6 inaashiria kwamba hili ndilo lilikuwa chimbuko la ofisi hii ya shemasi, na pia kuzua haja yake, ukweli ambao uliendelezwa zaidi mtume Paulo alipokuwa akiandikia Timotheo katika Timotheo wa Kwanza.



“Mashemasi ni watu ambao wameitwa kwa njia ya kiroho na kuhitimishwa kuwa watumishi wa kanisa.”

### Wajibu na Majukumu ya Mashemasi


Kwa urahisi mashemasi ni watu ambao wameitwa kwa njia ya kiroho na kuhitimishwa kuwa watumishi wa kanisa. Mwanahistoria Adam Clarke, ambaye pia alikuwa mwanathiolojia, aliandika kuhusu mashemasi na kusema: “Ofisi ya shemasi katika kanisa la kwanza ilikuwa ni ya kutumika katika sherehe za *agape*, sherehe za upendo, ili kusambaza chakula na mvinyo kwa washirika wa kanisa; na pia ilikuwa na kazi ya kufanya matangazo kuhusu sehemu tofauti na masaa tofauti ya ibada za kanisa; na pia wajibu wa kutunza wajane, mayatima, wafungwa, na hata wagonjwa, watu ambao walitunzwa kutoka kwa hazina ya kanisa . . . ilikuwa ni jukumu lao kutunza maskini na pia hata wakati mwingine wakaweza kuhubiri” (*Mafafanusi ya Adam Clarke kuhusiana na Mathayo 20:26*).

### Wenye Kuwajibika kwa Maswala ya Kila Siku

Tukisema kwamba moja ya wajibu mkuu wa mashemasi ilikuwa ni ya kusimamia fedha za kanisa litakuwa ni jambo ambalo haliwezi kuleta ubishi. “Katika masinagogi ya kale ya Wayahudi kulikuwa na watu watatu ambao walipewa jukumu la kutunza maskini . . . ni kutokana na mfano huo ndiposa mitume wakapata wazo la kuchagua mashemasi katika kanisa la Kristo. Ni wazi kwamba mitume walikusudia mashemasi hao wafanye kazi kama hiyo iliyokuwa ikifanywa na viongozi hao watatu wa masinagogi (*Maandishi ya Albert Barnes kuhusiana na Biblia* katika Mitume sura ya 6).

(Endelea katika Ukurasa 8)

Mwanzoni, watu hao saba walipewa jukumu la kusimamia ugawaji wa chakula kwa maskini, na pia wakasimamia maswala ya kifedha ya kanisa. Lakini jinsi ambavyo miaka iliendelea kupita, ndivyo ambavyo majukumu ya mashemasi yaliendelea kukua katika makusanyiko ya Kikatoliki (na hata yale ya Kiprotestanti), lakini kukua



**“Shemasi wa kweli hatumiki tu katika mambo yanayohusu dunia hii, bali pia yeye huwa nguzo muhimu katika huduma ya kanisa huku akisaidia mahali pote palipo na hitaji.”**

kwa majukumu hayo kulifanyika kulingana na dhehebu tofauti tofauti na kwa njia ya kimwili. Ndugu Ed Wilson, mzee wa kanisa katika Kanisa la Mungu aliandika na kusema: “Si jambo muhimu kwetu kutoa msururu wa majukumu na kazi ambayo shemasi anastahili kufanya. Hii ni kwa sababu wajibu wa mambo ya kiroho na wa mahitaji ya kila siku ya washirika ni mambo ambayo yanaingiliana kwa urahisi, bila ubishi wowote, kwa sababu chimbuko la majukumu yote ni moyo ambao ni safi, moyo ambao lengo lake kuu ni kufanya huduma ya aina yoyote ile kanisani.” Basi tunahitaji kuwa waangalifu sana tukijaribu kuonyesha wajibu zingine ambazo zinatakiwa kufanywa na ofisi hii; lakini pia ni kweli kwamba kuna vipengele vya ofisi hii (vya kimawazo na vya mambo ya kila siku maishani) ambavyo hata ingawa havijatajwa katika Maandiko kwa kweli vinalingana na ujumbe wa jumla wa Biblia.

Ofis ya shemasi ni ofisi ya utumishi, na kuna majukumu mengi ya maisha ya kila siku ya kanisa ambayo yanaibuka kila wiki kanisani na ambayo yanahitaji kusimamiwa vyema katika makusanyiko ya kanisa (utunzaji wa kanisa, uangalizi wake, utunzaji wa vipaza zaudi n.k). Wakati mwingi kazi hizi huweza kufanywa na washirika wa kawaida kanisani, lakini mara nyingi mtu

anayesimamia kazi yenyewe ni mmoja wa mashemasi wa kanisa. Ni kazi ya mashemasi kusimamia pesa za kanisa, na pia kusimamia utoaji wa hiari wa kusanyiko la kanisa. Pia ni wajibu wa mashemasi kutangaza mahitaji yaliyoko kanisani, na kuhakikisha kwamba sadaka za Wakristo zinachukuliwa kwa njia yenye utaratibu bora ili kukutana na mahitaji ya kawaida ya kanisa, na pia kwa ajili ya kuwasaidia watu, na hasa kwa lengo la kusaidia huduma yote ya kanisa. Pesa zote za kanisa zinahitaji kugawa kwa njia ya haki, na ambayo inalingana na ukweli. Wachungaji wengi na makusanyiko mengi ya kanisa yamewahi kupata madhara kutokana na mashemasi ambao hawakuwa waaminifu kufanya wajibu wao.

## Wasaidizi wa Huduma

Ni muhimu sisi kuzingatia kwamba watu wale watu saba katika Matendo ya Mitume sura ya 6 walichaguliwa na washirika wa kanisa, wakahakikishwa na mitume kazini

mwao, na pia wakapewa wajibu wa kusaidia mitume kubeba baadhi ya majukumu yao. Tukitumia mfano huo wa Matendo 6, ambao kwa kweli unastahili kuigwa, itakuwa dhahiri ni kwa nini tunasema kwamba kulingana na historia majukumu ya mashemasi yalikuwa zaidi ya maswala ya mahitaji ya kila siku ya kanisa. Shemasi wa kweli hatumiki tu katika mambo yanayohusu dunia hii, bali pia yeye huwa nguzo muhimu katika huduma ya kanisa huku akisaidia mahali pote palipo na hitaji.

## Uongozi wa Kiroho ambao Unaweza Kutegemewa

Kwa sababu mashemasi wanatakiwa kuwa wamehitimu kwa viwango vya hali ya juu kwa mambo ya kiroho, na pia ukweli kwamba washirika wa kanisa wanastahili kuwa na imani nao, mashemasi huwa sio tu viongozi kwa mahitaji ya kila siku ya maisha ya kanisa, bali hata kwa mambo ya kiroho. Wakati mchungaji hayumo kanisani tegemeo lake la usimamizi wa kanisa huwa kwa mashemasi. Wao basi huwa wamehitimu kiroho katika uongozaji wa ibada, na pia husaidia kudumisha utaratibu mwema kanisani. Wao husaidia kuongoza na kuendesha mikutano kanisani, na pia huwa ni kama daraja kati ya wazee wa kanisa na washirika wa kanisa. Mwandishi Adam Clarke alisema jambo muhimu kuhusiana na mashemasi “wakati mwingine wao huhubiri kanisani.” Mashemasi wengine huhudumu kuhubiri Neno la Mungu kama ambavyo shemasi Stefano na Filipino walifanya katika kitabu cha Matendo. Mashemasi waaminifu huziba pengo wakati kusanyiko la kanisa halina mchungaji, na hii ni kusema wakati huo wao ndio huwa na kazi muhimu ya kuhakikisha kwamba wazee wa kanisa wanadumisha ukweli na utakatifu wake kanisani.

Lakini baadaye ofisi ya shemasi ilifanywa kuwa yenye kufuata taratibu za kidunia na za kisiasa wakati ule kanisa Katoliki lilianza kukua na kusambaa. Ni jambo muhimu kuzingatia ukweli kwamba hapo mwanzo Kanisa Katoliki liliwakataza mashemasi kuwapatia washirika wake meza ya Bwana, lakini ikawaruhusu kubatiza watu ikiwa wazee wa kanisa hawakuwemo kanisani, ama kama kulikuwa na “hitaji kuu lililobidi jambo hilo kufanyika.” Maoni yangu binafsi ni kwamba kati ya watakatifu wa Mungu mashemasi wanaweza kusaidia aidha katika maswala ya ubatizo wa Wakristo au hata kushiriki Meza ya Bwana, wakati wao wameombwa kufanya hivyo na mzee wa kanisa. Kwa kweli jukumu kuu la kazi hii limo mikononi mwa wachungaji, lakini wao wanaweza kusaidiwa na mashemasi (ambao ni watumishi wa kanisa) wakati iko haja ya wao kufanya hivyo.

Sisi watakatifu tumeitwa ili kutumia mali na maisha yetu kwa ajili ya injili, kwa njia ya kuishi maisha ya utumishi. Lakini shemasi huwa na wito maalumu na hata nafasi maalumu ambayo anahitaji kujaza katika mwili wa Kristo. Lakini jambo hili si swala tu la cheo au heshima ya ofisi hiyo, bali hasa ni swala la mtu kutaka kumpendeza Mungu, kwa kufanya huduma ya kujitolea na ya kutumikia watu wa Mungu. Shemasi mwenye kutegemewa na ambaye pia ni mwaminifu huwa ni msaada mkubwa katika usaidizi kwa kazi ya huduma, na pia akiwa kama mtumishi wa Kanisa la Mungu. ■



## Je, nini tofauti kati ya mdhamini na shemasi?

Hata ingawa ofisi ya mdhamini haipatikani katika biblia na hata haijatajwa humo, kazi ya mdhamini wa kanisa ni kazi ambayo inaweza kukubalika kimaandiko, kwa sababu maana halisi ya wadhamini ni wasimamizi. Katika nchi nyingi bodi ya wadhamini, au bodi ya wakurugenzi, ni jambo ambalo linahitajika kisheria ili shirika au kampuni fulani ikubalike na kusajiliwa kulingana na sheria na ili ikubaliwe kuendesha shughuli zake. Wakati mwingi mdhamini huchaguliwa na kusanyiko la kanisa na kutumika katika wadhifa huo kwa muda wa miaka kadhaa kulingana na katiba ya kanisa hilo. Yeye huwa ndiye mwakilishi wa kanisa kwa mambo ya sheria, na kwa kulingana na matakwa ya sheria, yeye ndiye huwa na wajibu wa kusimamia majengo na mali ya kanisa, na hata anasimamia hati zote za kisheria zinazohusiana na kanisa, n.k. Wakati mwingi wadhamini huwa ndio husimamia ujenzi kanisani, na pia ndio ambao huchunga mambo ya kifedha ya kanisa. Zaidi ya hayo watu hawa ndio huwa wenye mamlaka ya kununua na kuzaa kwa jina la kanisa, ambalo sasa huwa ni shirika lililosajiliwa kulingana na sheria. Kuongezea, wadhamini ndio huwa na wajibu wa kuweka sahihi katika nyaraka zote za kisheria zinazohusu kanisa. Basi wadhamini na wakurugenzi huwa na wajibu muhimu wa kulidhamini kanisa, na inawabidi wao kuwa watu wanaoaminika na wakweli.

Wakati mwingi wadhamini hufanya kazi ya ushemasi, na majukumu ya ofisi hizi mbili hutangamana sana. Ofisi ya shemasi ni ofisi ambayo wajibu wake unatokana na Biblia, na ni ofisi ambayo ina umuhimu mkubwa wa kiroho katika maswala ya uendeshaji wa maisha ya kanisa. Basi mashemasi wanahitaji kuwa watu waliofuzu kwa kulingana na viwango vilivyowekwa katika 1 Timotheo 3, kama maofisa wanaotumika wa mambo ya kiroho kanisani, ilhali wadhamini wanatakiwa kuwa watu waliofuzu kulingana na matakwa ya sheria za nchi zao. Ndugu Ed Wilson ameandika na kusema, “Biblia imetoa viwango vya kuhitimu ambavyo vinatakikana kwa mashemasi, ilhali sheria za kanisa ndizo hutoa viwango vya kuhitimu vinavyotakikana katika maisha ya wadhamini wa kanisa.” Sheria fulani za makusanyiko ya kanisa zinasema kwamba mdhamini anastahili kuwa mtu ambaye amefuzu kuwa shemasi, lakini hili silo jambo ambalo hutakiwa na makusanyiko yote kwa jumla. Serikali zingine hutaka makanisa kuwa na wadhamini wanaotoka katika jamii ambazo makanisa hayo yanahudumu, kami vile kutokana na mawakili au waalimu waliomo katika jamii hiyo n.k. Basi kuna haja ya kutofautisha kati ya matakwa ya sheria, dhidi ya matakwa yanayotakiwa na serikali za kiroho ambazo ndizo huongoza mashirika ya kanisa. Kama vile mwandishi mmoja ameandika na kusema, “Shemasi hukutana na mahitaji ya watu, ilhali mdhamini hukutana na mahitaji ya mali na majengo ya kanisa.”

## Je, mashemasi wanastahili kuwekwa wakfu?

Kuweka wazee wakfu ni jambo ambalo linaonekana katika kanisa la Agano Jipya, na pia ni jambo ambalo linalingana na mafundisho ya Agano Jipya (tazama *Ukweli wa Injili* toleo la 33). Hata ingawa katika Agano Jipya hakuna sheria au kanuni inayohusu kuwekwa wakfu kwa wazee, kuna misingi ya mafundisho ambayo yanapatikana humo kuhusiana na swala hilo. Katika Matendo 6 baada ya wanaume (hao) saba kuchaguliwa, mitume waliwaombea na kuwawekea mikono. Wanathiolojia wamefanya mijadala mikubwa ya kama kwamba jambo hili lilikuwa ni sherehe kamili ya kuwekwa wakfu, au ilikuwa tu njia ya kuwahakikishia watu hao katika kazi hiyo ambayo walitakiwa kufanya. Ndugu Ostis Wilson ameandika kuhusiana na swala hili na kusema: “Watu hawa saba ambao walijazwa Roho Mtakatifu walichaguliwa na Kanisa na pia kuwekwa wakfu kwa ajili ya kazi hiyo (ya shemasi) na mitume, na wao walichukua usukani ili kuiongoza hali iliyokuwamo, na wakawezeshwa na hekima kutoka kwa Roho Mtakatifu ili kuongoza mambo hayo kwa njia ambayo ilikuwa sawa kabisa.”

Ukweli kwamba ofisi ya shemasi ni moja ya ofisi mbili tofauti kanisani, na pia tukizingatia ukweli kwamba kulingana na historia ya kanisa kuna mifano mingi ya watu kuwekwa wakfu kutumika katika ofisi hii, jambo hili linadhihirisha kwamba kuwekwa wakfu kwa mashemasi lilikuwa jambo ambalo linakubalika. Kuweka wakfu ni kitendo cha kuhakikisha na pia kuweka nguzo kanisani kuhusiana na wito wa Mungu katika maisha ya watu hao ambao watatumika kwa maswala ya mahitaji ya kila siku ya kanisa, na ni tangazo kwamba wao ni watumishi wanaotambuliwa kirasmi kanisani. Umuhimu wake haukuwa kwa cheo ambacho watu hao wangetumika bali “kilichokuwa muhimu ni washirika wa kanisa kuelewa kwamba hawa ndio watu ambao wanaweza kuwaenda kwao wakati wa shida na mahitaji” (Ed Wilson, 2020).

H.M. Riggle (mmoja wa wahudumu ambao ni wanzilishi wa Kanisa la Mungu) aliandika na kusema: “Katika kila kusanyiko . . . Bwana huwaita baadhi ya watu, na kwa njia ya Roho Mtakatifu Yeye huwahitimisha ili wawe wazee wa kanisa au maaskofu. Wengine nao anawaita ili waweze kufanya kazi ya mashemasi. ‘Yeye huita kila mmoja wa washirika katika mwili wake kulingana na jinsi inavyompendeza.’ Nalo kanisa hutambua wito huu kwa kuwawekea watu hao mikono, kama vile ambavyo mitume na wahudumu wa kale walivyofanya, kwa njia kuwatoa watu kwa kazi tofauti tofauti, wale ambao Bwana amechagua na kuwahitimisha. Jambo hili ndilo linajulikana kama kuwekwa wakfu. Mashemasi huchaguliwa na kuwekwa wakfu ili washughulikia mahitaji ya kila siku ya maisha ya kanisa” (*The Christian Church – Kanisa la Kikristo – 1912*).



JE, WAJUA?

Mchungaji wa Hamasi (Shepherd of Hermas –mwakani 150 BK) aliandika kuhusiana na mashemasi wapotovu na kusema:

“Wale ambao wana madoadoa ni mashemasi ambao wanatumia ofisi zao vibaya, na kuwaibia wajane na mayatima, huku wakijinufaisha kutokana na huduma ambayo walipewa kufanya” (Sim, IX, 26).



## MASKINI MWENYE HEKIMA

Yesu aliwaita wafuasi wake ili waishi maisha yenye urahisi na utumishi wa mmoja kwa mwenzake. Katika ulimwengu wa sasa wa dini ambako watu hushindana ili kupata vyeo, kuweza kutambulika, na hata kwa ajili ya kupata uwezo, hebu tafakari kuhusu hadithi hii ambayo ilisimuliwa na mfalme wa kale hapo Yerusalemu, na ambayo ilimhusu mtu mwenye hekima lakini ambaye pia alikuwa maskini.

“Palikuwa na mji mdogo, na watu ndani yake walikuwa wachache; akaja mfalme mkuu juu yake, akauhusuru, akajenga ngome kubwa ili kuupiga. Basi, kulionekana humo mtu maskini mwenye hekima, naye kwa hekima yake akauokoa mji ule lakini hata hivyo hapakuwa na mtu ye yote aliyemkumbuka yule mtu maskini. Ndipo niliposema, bora hekima kuliko nguvu; walakini hekima ya maskini hudharauliwa, wala maneno yake hayasikilizwi. Maneno ya wenye hekima yanenwayo taratibu husikiwa, zaidi ya mlio wake atawalaye katikati ya wapumbavu” (Mhubiri 9:14-17).



### Anwani

The Gospel Truth  
P. O. Box 2042  
Nixa, MO 65714  
USA

Email:  
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Laiti kungalikuwa ndani mwetu watu wengi zaidi ambao “ni maskini wenye hekima!” Ushindi katika vita vinavyotukabili pamoja na suluhisho za shida zetu hazipatikani kupitia kwa mtu ambaye anapaza sauti kujitangaza, wala si kupitia kwa mtu ambaye anatambulikana sana. Wakati mwingi hekima hupatikana kwa njia ya Mkristo wa kawaida, ambaye ni mwaminifu. Hata ingawa maskini huyu alidharauriwa na kupuuzwa, maneno yake ndiyo ambayo yalileta wokovu kwa jiji hilo. Yeye hakutangazwa kuwa ni shujaa wa mji, na hakuna heshima ambayo alipewa. Hata hakuna sherehe na karamu zilizofanywa ili kumpatia heshima. Na hamukuwa na mabamba au michoro mikubwa iliyoundwa kwa ajili ya ukumbusho na kumbukumbu zake kama mwokozi wa jiji. Watu wa jiji hili ambao mwanzoni walikuwa karibu kuangamizwa waliendelea na maisha yao ya kawaida, na mtu huyu maskini mwenye hekima akasahaulika.

Wakati mwingi kazi ya Mungu katika makusanyiko ya kanisa huweza kuendelea kupitia kwa ushindi ambao chanzo chake ni mwanaume au mwanamke maskini mwenye hekima. Kazi ya mshirika kama huyo haina heshima na hata haina vigelegele. Wakati mwingi majina ya watu hao hayatangazwi ili kutambua utumishi wao, hekima yao, au uaminifu wao; lakini bila wao mji huo huangamia. Huyo maskini mwenye hekima hakutambuliwa, lakini hata katika umaskini wake yeye alipeana hekima yake wakati ambao ilihitajika. Hebu hili liwe himizo kwa kila mtoto wa Mungu, kwamba asitafute heshima au mamlaka, lakini lengo lake kuu liwe kwamba katika umaskini wake aweze kumpendeza Bwana wake, huku akiendelea kutumia hekima yake ambayo haijatangazi, na hata kujipa nguvu za kuwatumikia watu wale wengine kanisani.

Enyi waume na wake maskini, ambao wako na hekima, na ambao wamo katikati mwetu, asanteni kwa upendo wenu, neema yenu, hekima yetu, na hata utumishi wenu. Tunawapenda na tunawafurahia. Mungu Mwenyewe na awabariki! ■